

ILIMANJARO



Ukimya, uoga, visasi unavyochangia ukatili kijinsia

Na Godfrey Mushi, MOSHI

STADI ya awali ya kuhusu ukatili wa kijinsia kańka mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, inaonyesha tamaduni ya ukimya na uoga wa kulipwa visasi ni mionganini mwa visababishi na matokeo ya ukatili wa kijinsia unaoendelea kutikisa katika jamii ya ukanda huo.

Akizungumzia stadi hiyo, mratibu wa mradi wa kukuza usawa wa kijinsia kwa kutumia elimu ya haki za binadamu Shirika lisilo la kiserikall la Tusonge Consolatha Kinabo, alisema mbalina wa kuwapo kwa visasi, kuna jambo la uhaba wa mifumo ya ulinzi pamoja

Alikuwa akitoa mrejesho kuhusu stadi hiyo, wakati wa uzinduzi wa awamu ya pilli ya mradi huo uliofanyika katika Manispaa ya Moshi na kujumuisha wadau zaidi ya 50 kutoka mashirika mbalimbali.

"Visababishi na matokeo ya ukatili wa kijinsia tumeona kwamba mtoto wa kike anapata ujauzito, maisha yake ya baaadaye huandaliwa kuwa mama wa nyumbani ila kwa kijana aliyehusika na ujauzito huo huendelea kupata fursa za

kufanikiwa kimaisha.

"Sababu zinazochangia ni tamaduni ya ukimya na uoga wa visasi, uhaba wa mifumo ya ulinzi, umaskini, unyanayapaa wa kijamii, uelewa duni wa haki za binadamu na usawa wa kijinsia. Visababishi ni mila potofu na tamaduni zinazokandamiza kutokana na jinsia."

Mkurugenzi Mtendaji wa Tusonge, Agnatha Rutazaa, akiwasilisha matokeo hayo kwa wadau na Kansela Mkuu wa Ushirikiano na Maendeleo wa Serikali ya Canada, kuitia ubalozi wake nchini Tanzania, Gwen Walmsley, alisema aina za ukatili zilizoalnishwa na wanajamii ni ukatili wa klingono kwa watoto, rushwa ya ngono na ukatili wa kisaikolojia unaohusisha matusi na vitisho.

Alitaja aina nyingine kuwa ni ukatili wa kiuchumi kama kutopewa elimu, fursa, urithi, ardhi na masuala ya ukatili wa kimwili ikiwamio vipigo na kujeruhija na silaha. Yamo pia masuala ya mila potofu kama ndoa za utoroni, ndoa za kulazimishwa na ukeketaji.

Hata hivyo, wakati anazindua awamu ya pilii ya mradi huo unaotekeliza kuanzia mwaka 2019/2024, Kansela Gwen alisema,

changamoto ya ukatili wa kijinsia ipo nchini Tanzania na kwamba kwa sasa Tanzania inashika nafasi ya 130 kati ya 160 katika masuala ya haki na usawa wa kijinsia.

"Bado changamoto zipo katika masuala ya usawa wa kijinsia, kwa sababu Tanzania ina uwakilishi mzuri katika utawala, wakati jambo hili linaanza Tanzania illikuwa na Spika wa Bunge mwanaamke Anne Makinda na sasa tuna Makamu wa Rais ambaye ni mwanaamke (Samia Suluhu Hassan) na mengi ambayo tunayaona kwa wanawake wa Tanzania wamechukua nafasi za uongozi ambazo zinatia hamasa watoto wa kike Tanzania nzima," alielez.

"Naomba niwapongeze Tusonge, Equitas na mashirika mengine kwamba ni matumaini yetu mambo ya msingi kama haki za binadamu na ukatili wa kijinsia yataenda kutatuliwa kwa kupatiwa usumbuzi wa kudumili."

Kansela Gwen alisisisitiza kuwa kwa jinsi Tanzania inavyojitahidi kuzallsha kwa kifwimgo cha kina cha kati, anaamini tafsi haliwezi kuwaacha wanawake nyuma, hivyo ni lazima wahitaji mchango wa wanawake ili kufikla malengo hayo.